

Learning by Ear 2011 – Mikinzano na utatuzi – “Mizozo na utatuzi – “Palipo na wazee”
KIPINDI cha 1: “Ardhi yangu, maisha yangu”
AUTHOR: Chrispin Mwakideu
EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo

Narrator (m/f 30-40)

SCENE ONE : MORNING AT KIJANI VALLEY

- **Masambo (m, 50)**
- **Nina (f, 40)**
- **Lawi (m, 20)**
- **Gulu (m, 17)**

SCENE TWO : MORNING AT THE MITUMBA'S HOUSE

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f,17)**

SCENE THREE: OUT IN THE GRAZING FIELDS

- **Lawi (m, 20)**
- **Gulu (m, 17)**

SCENE FOUR: LELA, SHANI AND MITUMBA ON THEIR FARM

- **Mitumba (m, 50)**
- **Lela (f, 20)**
- **Shani (f, 17)**

Msimulizi

UTANGULIZI:

Salamu, na karibuni katika kipindi kipyua makala ya Noa bongo! Jenga maisha yako. Wakati huu, tutaangazia tatizo la muda mrefu barani Afrika ambalo

limekuwa changamoto kubwa kwa bara hilo, nalo ni **“Mizozo na utatuzi”**. Kaa nasi kwa vipindi kumi vijavyo wakati tutakutana na Masambo na Mitumba, viongozi wa familia mbili, kutoka makabila tofauti, lakini wanaishi pamoja katika sehemu iliyo na rutuba ya bonde la Kijani. Hawa wawili watakumbana na mikinzano mingi, kweli watapata suluhu ya kudumu na kuishi kwa amani? Yote haya yamo katika mchezo wetu huu wa redio uitwao, **“Palipo na wazee”**. Masambo na jamii yake ni wafugaji ilihali Mitumba na familia yake ni wakulima. Hiki ni kipindi cha kwanza kinachoitwa, **“Ardhi yangu, maisha yangu”**. Ni asubui mbichi katika bonde la Kijani, familia zote mbili ziko tayari kuanza siku yao.

SCENE ONE: MORNING AT KIJANI VALLEY

<p>1. SFX: VILLAGE MORNING AMBIENCE (as it is a pastoralist village: cicada chirping, birds)</p>

- 2. MASAMBO:** **(calls out)** Lawi! Gulu! Amkeni! kumekucha.
Wakati wakulisha ng’ombe ndio huu, mukilala jua litakausha nyasi nzuri za mifugo yetu.
- 3. GULU:** **(sleepy voice)** Baba, bado giza li tii huko nje, tutawaongoza vipi ng’ombe kama hatuoni twendako.
- 4. LAWI:** Ndio, mbali na hayo, nyasi zimeadimika huku siku hizi.
- 5. MASAMBO:** Hamwishi kulalamika, nyinyi wawili, hebu amkeni!
Kuwe na giza au mwangaza, kuwe na nyasi au hamna, hao ng’ombe ni sharti wakashwe. Bila

ng’ombe

6. GULU/LAWI: **(finish sentence)** Hatuna mbele wala nyuma! Kazi wala bazi!

7. NINA: Masambo, mumewangu. Kwanini tusiwauze hao ng’ombe, alafu tununue kiwanja, tujenge nyumba na...

8. MASAMBO: **(Furious and bitter)**Tuishi kama jirani yetu Mitumba? Hapana! Tunafuata tamaduni za mababu zetu, tangu jadi wao ni wafugaji. Kwanini leo hii mimi ndiyo nigeuze mila zetu? Mwataka laana za mababu zinipate?

9. LAWI: Sawa baba, tutakwenda. **(to Gulu)** Gulu, twende.

10. NINA: Lakini mumewangu Masambo, basi waache watoto angalau watie kitu tumboni ndio kisha waende.

11. MASAMBO: Hapana! Hakuna mtu yeyote atakaye kule humu ndani kabla ng’ombe hawajala.

12. SFX: COWS MOOING

13. GULU: **(leading cows)** Pssssh! Pssssh!..nje! Twende huku, huku. Pssssh

14. MSIMULIZI: Katika bara Afrika, jamii nyingi za wafugaji, ng’ombe ndio ngome yao ya maisha, ng’ombe ni ishara ya kuwa na mali, ni kama kulinganisha na kuwa na akaunti benki yenye pesa furi. Ng’ombe aweza kulipia mahari, na kutumiwa kufanyia biashara na kupata bidhaa nyengine. Maziwa, nyama, ngozi, hata mavi ya ng’ombe yalitumiwa

kukuzia chakula, kutengezea bidhaa nyengine, au hata kwa ujenzi. Masambo alikulia mazingara haya. Jirani kando na hapo, Mitumba aliishi na binti zake wawili, Shani na Lela walikuwa tayari wameamka na wanapata kiamsha kinywa.

SCENE TWO: MORNING AT THE MITUMBA'S HOUSE

15. SFX: COCK CROWING IN THE MORNING

- 16. SHANI:** Lela, Si uolewe. Utazeekea hapa nyumbani!
- 17. LELA:** **(agitated)** Shani!, utaacha lini kunikera na suala la mimi kuolewa?
- 18. SHANI:** Nyanya yetu aliolewa akiwa na miaka 18.
- 19. LELA:** Kwa hivyo? Una miaka 17 sasa, je, unaolewa mwaka ujao? Mambo yamegeuka siku hizi!

20. SFX: OPENING OF DOOR

- 21. MITUMBA:** Wanangu, kelele na asubui ni za nini? Jogoo ndiyo mwanzo yuwawika, jua latoka sasa, ni siku mpya. Ugomvi ni wa nini?
- 22. LELA:** **(Still angry)** Ni Shani, Saa zote ananihimiza niolewe. Ni kama ambaye hataki kuniona hapa nyumbani kesho!
- 23. SHANI:** Yalikuwa ni maoni.
- 24. MITUMBA:** Mimi nina maoni mazuri zaidi, malizeni kiamsha kinywa, mwende shambani. Mahindi yameshika

vizuri, na kwekwe pia nazo. Kama mwataka tuvune vizuri basi ni lazima tuyalimie kwekwe mahindi.

25. SHANI: Ndio baba.

26. LELA: Ni sawa baba.

27. MITUMBA: Kitu chengine, kuhusu mada yenu ya ndoa. Munaweza kuolewa na yeyote mumtakae, binti zangu, yeyote, ila tu siye wa jamii ya Masambo. Kwa sababu hao ni wa kabila la Torube. Kama mujuwavyo, sisi, ni wa Koroma, na tuna vita vya jadi na wao! Sawa binti zangu. Niko nje nawasubiri.

28. SFX: DOOR CLOSED

29. SHANI: Hiyo inamaanisha huwezi kuolewa na Lawi na mimi sitaolewa na Gulu.

30. LELA: Shani, una kichaa kama ulidhani hiyo inawezakana.

31. MSIMULIZI: Torube na Koroma ni jamii za kabila mbili ambazo zimetumia ardhi pamoja kwa miaka mingi. Bali kila wakati walikuwa kwenye mikinzano na chuki. Je, kuna uhasama mpya unatokota kati ya jamii za Masambo na Mitumba? Letu ni sikio. Kwa sasa, katika sehemu za malisho, Kaka wawili Lawi na Gulu wako uwanjani, wanalisha ng’ombe zao – ijapo wenyewe matumbo yanawavuta kwa njaa.

SCENE THREE: OUT IN THE GRAZING FIELDS

32. SFX: COWS MOOING, GOATS, SHEEP BLEATING E.T.C

- 33. GULU:** Lawi, Nasikia njaa. Tumkamue ng’ombe mmoja, au tuchinje moja, tuile. Wasemaje?
- 34. LAWI:** Gulu, tukijaaribu kukamuwa ng’ombe hata tone moja la maziwa ujuwe baba atajuwa licha ya kuchinja, wakati mwengine, hufikiria baba anawajuwa ng’ombe hawa vizuri hata kutuliko sisi.
- 35. GULU:** **(jeering)** Aah... Wewe ni fisi tu, ni hivyo!
- 36. LAWI:** Gulu, umeniitaje?
- 37. GULU:** Mwoga! Kwani?
- 38. LAWI:** **(furious)** Niombe msamaha, Gulu, tena sasa hivi! Au sivyo....
- 39. GULU:** Sivyo nini? Wewe ni mwoga mwenye njaa, kwani...
- 40. LAWI:** **(Stressful)** Mimi ni mpiganiaji wa Torube! Mimi si mwoga!
- 41. GULU:** Pia mimi karibuni nitakuwa mpiganiaji wa Torube. Lakini unajuwa nini, Lawi? Najihisi kama wao.
- 42. LAWI:** **(charging)** Hakuna mtu yeyote amesubutu kunizungumzia hivyo! Unasikia wewe mkosa adabu!

43. SFX: FIST HITTING FACE

44. GULU: (cries out) Awww! Utajuta kunipiga, Lawi!

(Gulu and Lawi act out as if engaged in a real tight fight)

45. LAWI: Wewe! Tuone nani atakayeibuka hapa na kicheko!
Hmm, Utaweza hii! Nitakunyonga macho yakutoke
kama panya aliyebanwa kwa mlango.

46. GULU: (Breathing in difficulty) Arrrgh arrgh!

47. SFX: GRASS BEING UPROOTED

48. GULU: (screaming in difficulty) Niko na nyasi! Acha vita!
Niko na nyasi!

49. LAWI: Bahati yako umeng’oa nyasi, ningelikumaliza.
Lakini bahati yako. Vita vimekwisha, tusahau.
Tumepatana.

50. GULU: (now breathing normally) Hivyo tu? Kwanini?

51. LAWI: Kwanini nini?

52. GULU: Mbona nyasi na sio mchanga au mawe au nywele?
Kwanini sisi wa Torube huwacha kupigana mara tu
mtu ang’owapo nyasi?

53. LAWI: Kwa wa Torube, nyasi ni takatifu. Ni ishara ya uhai,
zinalisha ng’ombe na baadae ng’ombe nao
wanatulisha sisi. Uhusiano huu unatukumbusha
kuwa tu wamoja. Tumetoka tumbo moja,
tumenyonya maziwa ya titi moja. Utafunzwa haya
yote ukifika miaka kumi na nane.

54. GULU: Nitakapokuwa mpiganiaji.

55. LAWI: Hayo ni baadhi ya mafunzo. Twende tutafute nyasi nzuri pahala pengine.

56. SFX: COWS MOOING

57. GULU: Unafikiri kutanyesha hivi karibuni, Lawi? Au tutahitajika tuhame tena?

58. LAWI: Huu ni msimu wa mvua. Hatutahama. Hii ardhi ni yetu, haya ni maisha yetu.

59. GULU: Lakini inawezekana vipi kuwa mimea ya familia ya Mitumba daima imenawiri na iko kijani licha ya kuwa mvua imeadimika?

60. LAWI: Ni kwa sababu wanavuta maji kutoka mtoni. Hiyo ndiyo sababu kuu kwanini hatuelewani nao. Kwa sababu ng’ombe wetu sasa wanapungukiwa na maji ya kunywa.

61. GULU: Kama ni hivyo, kwanini na sisi tusiwavutie ng’ombe wetu maji ya mto wakanywa?

62. LAWI: Kwanini? Mtu huiba kile ambacho siyo halali yake. Vyote unavyoviona hapa, miti, milima, mito, vyote ni vyetu. Tulipewa na Mungu, walikabidhiwa mababu zetu. Utajifunza hayo ukiwa....

63. GULU: **(Cuts him short)** Nimefika miaka kumi na nane. Najuwa... najuwa.... **(To the cows)** Pssh pssh..

64. SFX: COWS MOOING AGAIN AND AGAIN

65. NARRATOR: Mmojawapo ya chanzo cha mikinzano Afrika ni utetezi wa rasilimali. Jamii ya Masambo na Mitumba tayari washaanza vita - ingawa si vya ana kwa ana - ni vya maji ya mto ulio karibu yao. Vita hivi vitaendelea kukua? Zidi kusikiliza. Lakini sasa tujunge na Shani akiwa na Lela shambani kwao.

SCENE FOUR: LELA, SHANI AND MITUMBA IN THEIR FARM

66. SFX: GROUND BEING PLOUGHED BY HOES, RAKES ETC

67. MITUMBA: (Breathing hard) Efu! Nahitaji kupumzika, binti zangu. Leo, ambavyo nimefika miaka 50, sina ari tena na nguvu kama nilivyokuwa kijana.

68. LELA: Pia mimi nimechoka.

69. SHANI: Mimi zaidi..

70. MITUMBA: Sawa. Basi tupumzikeneni tupate kunywa maji.

71. SFX: WATER BEING Poured INTO GLASSES / CUPS.

72. MITUMBA: Asante.

73. SFX: GULPING OF WATER (studio)

74. MITUMBA: Ahh..Sasa afadhali. Nilikuwa na kiu sana.

- 75. SHANI:** Baba, kabila letu limeweza kuishi vipi katika bonde la Kijani kwa miaka yote hiyo, limeishi vipi na wa Torube na wengineo?
- 76. LELA:** Shani, huu sio wakati muafaka wa maswali. Tunapumzika tujiburudi nafsi!
- 77. MITUMBA:** La, hilo lake ni swali zuri, Lela, la linahitaji jibu zuri pia.
- 78. LELA:** Kumradhini, Narudi sasa hivi.
- 79. MITUMBA:** Lela, tutakusubiri. Kwa sababu haya pia ni muhimu kwako.
- 79b: LELA** Sawa naja hivi punde.

80. SFX: LELA WALKING THROUGH A MAIZE FIELD

- 81. LELA:** **(screams from far away)** Baba! Baba! Baba!
- 82. MITUMBA:** Nini? Lela umefanyika nini?

83. SFX: SOMEONE RUNNING THROUGH A MAIZE FIELD

- 84. LELA:** Tazama! Wamefanya tena!

85. SFX: WATER RUNNING IN A RIVER

- 86. SHANI:** Baba hii ni mara ya tatu kwa juma moja wametufanyia hivi . Baba, watazoea kutufanyia hivi...

87. MITUMBA: (totally enraged) Wanacheza na moto, na daima!
Wanaocheza na moto wanatafuta kuchomeka!

OUTRO:

Huku Mitumba akikunja ngumi na kuuma meno kwa hasira, tunatamatisha kipindi cha kwanza cha mchezo wa redio kuhusu mikinzano na utatuzi. Ni kipi hicho kilichowatifua Mitumba na binti zake? Watachukua hatua gani? Lawi na Gulu watakapokosa nyasi, watachukua hatua gani? Kwa haya na mengine usikose kipindi kifuatacho cha “ **Palipo na wazee**”

Kusikiliza kipindi hiki tena, tembelea tovuti zetu www.dw.de/kiswahili

Mpaka tutakapokutana tena, kwaheri.